

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI KUHUSU UHAMISHAJI WA WANAFUNZI KWA VYUO VILI VYOSITISHIWA MASOMO NA KUAGIZWA KUHAMISHA WANAFUNZI WANAOENDELEA NA MASOMO

Itakumbukwa kwamba, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) mwezi Septemba 2018 ilifanya maamuzi yafuatayo kwa baadhi ya vyuo kutokana na changamoto za ubora zilizobainishwa katika ukaguzi uliofanywa na Tume:

- a) Kufuta Vituo viwili (2) vya Vyuo Vikuu na kuamuru wanafunzi wote wanaoendelea na masomo wahamishwe;
- b) Kusitisha utoaji wa mafunzo katika Vyuo Vikuu vitano (5) na kuamuru wanafunzi wote wanaoendelea na masomo wahamishwe; na
- c) Kuzuia udahili wa wanafunzi wapya katika Vyuo Vikuu saba (7).

Maamuzi haya yalizingatia umuhimu wa kuwa na wahitimu wenye kukidhi viwango bora vya elimu kitaifa na kimataifa kwa manufaa yao binafsi, jamii zao na Taifa kwa ujumla.

Vyuo vyote vilivyoagizwa kuhamisha wanafunzi vinatakiwa kutekeleza maelekezo ya Tume kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kuhamisha taarifa zote za kitaaluma za wanafunzi kwenda katika chuo anachohamia mwanafunzi haraka iwezekanavyo kabla ya kuanza kwa muhula wa kwanza wa masomo kwa mwaka 2018/19.

Pia Tume inawataka wanafunzi wote kufuata maelekezo na taratibu zilizowekwa ili kukamilisha utekelezaji wa agizo hili kwa haraka na kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

Tume inasisitiza vyuo vyote vilivyoagizwa kuhamisha wanafunzi kuzingatia maridhiano baina yake na vyuo wanavyohamia wanafunzi ili kuepusha migongano isiyokuwa ya lazima.

Aidha, Tume imesikitishwa na mkanganyiko uliojitokeza katika kuhamisha wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira (JOKUCo) kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Tume inaushukuru Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa jinsi walivyotatua changamoto hii na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliohamishwa wanapata hifadhi na malazi kwa muda wakati taratibu nyingine za uhamisho zikiendelea.

Imetolewa na

**KATIBU MTENDAJI**

**29/10/2018**